



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 18 Mei, 2016.

Kikao kitaanza saa 3.00 (Tatu) asubuhi
na dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 27 Juni, 2015.

Waziri wa Fedha na Mipango:

Hotuba ya Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Mwaka 2016/2017.

Hotuba ya Kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2016/2017.

II. MASWALI:

WIZARA YA NCHI, OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS:

49. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:

Ahadi zinazotolewa katika Baraza la Wawakiishi na Mawaziri wananchi huwa wanazisikia na Waziri anaetoa ahadi anapaswa kutekeleza ahadi yake kwa wakati.

- a) Ahadi zinazotelewa na Mawaziri hupitiwa mara ngapi kwa mwaka kujua ahadi gani zilizotekelezwa na ambazo hazijatekelezwa kwa manufaa ya wananchi.
- b) Je, ni hatua gani Ofisi ya Makamo wa Pili huchukua pale Waziri ametoa ahadi kupitia chombo hiki na baadae kushindwa kutekelezwa kero kubakia kwa wananchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:

10. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani): - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Zinatangazwa nafasi za ajira Serikalini zinakuwa na masharti magumu wakati kazi nyengine hata vijana waliomaliza F. III wanaweza kufanya.

- a) Je, Serikali haioni kuwa vijana hawa nao wanahaki ya kufanya kazi kwa sababu kazi nyengine hazihitaji elimu kubwa, zinahitaji hekima na busara na utulivu wa mtu.
- b) Je Serikali ina mpango gani wakusaidia wasomi wenye elimu ndogo kupata ajira hizo.

WAZIRI WA HABARI, UTALII, UTAMADUNI, NA MICHEZO:

5. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni, na Michezo:

Serikali ya SMZ chini ya Kiongozi imara Dkt. Ali Moh'd Shein inastahiki pongezi kwa kuamua kuujenga upya Uwanja wa Mao lakini mbali na maamuzi hayo mazuri.

- a) Je, ujenzi wa uwanja huo utanza lini na kumalizika lini.
- b) Je, gharama ya ujenzi wa uwanja huo utakuwa kiasi gani hadi kumalizika kwake.

WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO:

15. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Wanawake wengi sasa hivi wameamka kujijiri wenyewe pamoja na kujiunga katika vikundi mbali mbali ikiwemo "Saccos" na vikoba lakini vikundi hivi baadhi ya Shehia vinakufa haraka kwa kukosa elimu ya ujasiriamali.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hawa ili waweze kuviboresha vikundi hivi.

WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA:

1. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Tatizo la maji katika Jimbo la Kijitoupele ni kero kubwa kwa wananchi katika baadhi ya maeneo kama vile Kwarara, Kwarara kwa Madina, Taveta, Tomondo Uzi, Meli nne, pamoja na Meli Nne Uzi.

Kwa kuwa tatizo hilo lipo kwa muda mrefu sasa, Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwapatia maji wananchi wa maeneo hayo.

WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI:

13. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kilimo ndio uti wa mgongo na wananchi wengi hivi sasa wamekuwa na mwamko wa kulima lakini wanalima kwa mazoea tu ukilinganisha na nguvu zinazotumika na wanachovuna.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wakulima hao matrekta na pembejeo za kutosha.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwamba Baraza hili lifikirie na kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Mwaka 2016/2017.

Kwamba Baraza hili lifikirie na kuyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2016/2017.

Zanzibar,
18 Mei, 2016.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.